Jarida la Wamama wa Maombi Kimataifa

Kanisa la Umoja Pentekoste- Huduma ya Wamama

Agosti 2014

Wamama wa Maombi Kimataifa

Sisi ni nani… Wamama wa Maombi wa Kimataifa imeundwa na wanawake duniani kote tangu mwaka 1999. Wanawake hawa hukutana Jumatatu ya kwanza ya kila mwezi kuungana katika maombi kwaajili ya watoto wao na watoto wa kanisa la mtaa na jamii.

Dhamira yetu ... Nia yetu ni kuhifadhi kiroho kizazi hiki na zaidi, pia kurejesha kiroho vizazi vilivyopita

Haja yetu ... Wanawake watakaojiunga pamoja Jumatatu ya kwanza ya kila mwezi kuombea watoto wao**.**

Vipaumbele vitatu vya Maombi ...
1. Wokovu wa watoto wetu (Isaya 49:25; Zaburi 144:12, Isaya 43:5-6).
2. Kwamba wachukue umiliki wa imani katika umri wa kuwajibika (I Yohana 2:25-28; Yakobo 1:25).
3. Kwamba waingie katika huduma ya mavuno ya Bwana (Mathayo 9:38).

Sala ya kurejea shule

Debbie Akers

Mwezi huu watoto wetu wengi watarudi madarasani kuelimishwa na kufunzwa stadi za jamii. Hili ni jambo jema na lenye umuhimu sana. Lakini zaidi na zaidi shule zetu zinazidi kuwa maeneo ya hatari.

Mwaka uliopita shule ya mjukuu wangu iliwekwa kwenye lockdown kwasababu mtu asiyejulikana alivunja kiwango cha juu cha usalama wa shule hiyo. Vyombo vya habari vimejaa matukio kama haya duniani kote, baadhi na matokeo ya kutisha.

Kila nikisikia moja ya hali hizi, ninakumbushwa jinsi mama yangu alivyokuwa akitufanya tupige magoti kwa ajili ya sala fupi kila siku kabla ya kuondoka kwenda shule. Maombi ni ya muhimu na yana NGUVU!

Nawakaribisha akina mama wote duniani kuungana nami kila siku na kupumua sala ya usalama kwa ajili ya watoto wetu wakiwa wanaelekea shule mwaka huu ujao. Nahisi Mungu ameweka hili moyoni mwangu na ninajua Yeye ana uwezo wa kulinda na kuwaweka watoto wetu dhidi ya madhara!

Mwenyezi-Mungu atakukinga na baya lolote; atayalinda salama maisha yako. -Zaburi 121:7

‘Mwenyezi-Mungu awabariki na kuwalinda; Mwenyezi-Mungu awaangalie kwa wema, na kuwafadhili; Mwenyezi-Mungu awaoneshe wema wake na kuwapa amani.’ -Hesabu 6:24-26

Mlee Mtoto

Adena Pedigo

Mei 31, 2014, mtoto wangu wa mwisho alihitimu sekondari. Mume wangu, Tim, alipewa heshima ya kuzungumza katika sherehe ya kuhitimu kwake. Katika moja ya mifano yake alisema, "mtoto kutoka chekechea hadi daraja la kumi na mbili atatumia siku 2,160, au masaa 18,900, ya maisha yake akifundishwa shuleni."

Wazo hili lili nipiga gumzo ndani yangu- masaa18, 900 ya kujifunza lugha, hisabati, sayansi, historia, fasihi, sanaa, muziki, na kadhalika. Lilinifanya niulize swali, "Je, ni masaa mangapi nimetumia kumfundisha mambo ya Mungu?" Nimewapeleka watoto wangu kanisani. Tumekuwa na ibada za familia, nyakati za sala, na mazungumzo kuhusu mambo ya Mungu na jinsi ya kuwa Mkristo mwema tangu walipozaliwa. Lakini, kama ningeshaanza hata kujishughulisha masaa 18,900 kwa watoto wangu, Je, ningefanya zaidi?

"Mpendeni Mwenyezi-Mungu, Mungu wenu, kwa moyo wenu wote, kwa roho yenu yote na kwa nguvu zenu zote. Wekeni mioyoni mwenu maneno hayo ninayowaamuru leo: na kuwafundisha kwa uangalifu watoto wenu. Mtawasimulia muwapo mnakaa nyumbani au mlipo safarini au mnapolala au mnapoamka. "
(Kumbukumbu la Sheria 6:5-7).

Tunaishi katika wakati unaobidi kuwaombea, na kuwafundisha zaidi, watoto wetu kuhusu mambo ya Mungu. Hatuwezi kuwategemea tu viongozi wa kanisa kufundisha watoto wetu mambo ya kiroho. Kama wazazi, ni lazima tuwafundishe watoto wetu. Ni lazima tujitolee muda kwa ajili ya ukuaji wao wa kiroho.

Watoto wa leo wanataka jibu la swali, "Kwa nini?"

- Kwa nini tunaamini kwamba kuna Mungu mmoja tu?
- Kwa nini Matendo 2:38 ni msingi wa imani yetu?
- Kwa nini utakatifu ni muhimu?

Tunashauriwa, "Muwe macho; kesheni! Maana adui yenu, Ibilisi, huzungukazunguka kama simba angurumaye akitafuta mawindo." (I Petro 5:8). Sitaki shetani awachukue watoto wangu na nina uhakika hautaki awachukue wako pia. Ni wajibu wetu kuwafundisha hatari na hasara za kuishi maisha bila ya Mungu katikati yake. Ni lazima tuwe na bidii katika kufundisha, kushauri, na kuomba kwa ajili ya watoto wetu.

"Mlee mtoto" (Mithali 22:06) ni maneno yanayo rushwa juu juu mara kwa mara, lakini hubeba wajibu mkubwa kwa wazazi wote. Malezi ni safari ndefu.

Tuta waona watoto wetu wakipata stashahada, wakienda kufunga ndoa, na wakitimiza malengo mengine mengi maishani. Lakini ushindi mkuu kwa wazazi ni kuweza kusema, pamoja na mtume Yohana, "Hakuna kitu kinachonifurahisha zaidi kuliko kusikia kwamba watoto wangu wanaishi katika ukweli." (III Yohana 4).

Kumbuka: Adena Pedigo ni Rais wa Wizara ya Wamama ya Indiana. Yeye na mume wake, Tim, ni wachungaji wasaidizi wa Calvary Tabernacle Indianapolis, linalosimamiwa na Mchungaji Paul D. Mooney. Amebarikiwa na watoto wawili, Maci na Georgeon Pedigo.

Darla Dillon

Nimeitwa kufanya kazi nyingi katika maisha yangu, lakini hakuna la muhimu kama kulea watoto wangu. Mtoto wetu wa kwanza alipozaliwa, alikuja bila "mwongozo" au orodha ya "jinsi ya". Ilibidi mimi na mume wangu twende siku moja baada ya nyingine, changamoto moja baada ya nyingine, na kujifunza kadri tukienda.

Maandiko yanatuambia katika Mithali 22:6, "Mfunze mtoto namna ya kuishi vizuri, naye hatasahau njia hiyo hata uzeeni." Katikati ya kuzaliwa na utu uzima tuna muda mfupi wa kuwafundisha watoto wetu kumuelewa Mungu na mambo ya Mungu, kuwapa maisha yao sura ili, kama sio papo hapo, wakati fulani watamtumikia Mungu.

Kila siku lazima tutumie vizuri muda huu mfupi tuliopewa. Ni lazima tushughulikie mambo muhimu kwanza, na kuruhusu mengine kufuata kama yawezavyo. Kamwe hatutapata muda wa kufanya kila kitu tunachopenda, hivyo ni lazima kuchagua mambo ambayo yataathiri maisha yao zaidi.

Wakati kuna mambo mengi tunaweza kutaja ambayo ni ushawishi kwa watoto wetu, naamini moja ni muhimu zaidi. Ni somo tunalofundisha kwa maisha yetu.

Imesemekana, "matendo yetu husema kwa sauti zaidi kuliko maneno yetu." Hii ni kweli. Kadri watoto wetu wanavyokua na kukomaa, tunawaelimisha kuhusu mambo mengi ya maisha ya Kikristo - mahudhurio ya kanisa, neno la Mungu, shule ya Jumapili, maisha ya kumcha Mungu, na mengineyo. Wao watapima wanayo sikia na yale wanayoona nyumbani. Tunathibitisha kile wanachofundishwa kwa kuwapa mfano kila siku machoni mwao.

Namna tunazo onyesha vigezo hivi, mafundisho, na vipaumbele hutuwezesha kutoa mafunzo bora. Tunaonyesha hivi kupitia:

- Kudumisha uhusiano wa karibu, na wa kibinafsi na Mungu.
- Kupenda neno la Mungu.
- Kuonyesha umuhimu wa maombi.
- Kufanya mahudhurio ya kanisa na mambo ya Mungu kipaumbele.
- Kuheshimu kanisa, uongozi wake, na watu wake.
- Kufanya maamuzi sahihi katika mambo tunayofanya (au tusiyo fanya).

Tuna yataathiri maisha ya watoto wetu kwa njia nyingi. Kati ya hizi, naamini somo muhimu zaidi ni lile tunalofundisha kupitia maisha yetu!

"Nyinyi wenyewe ni barua yetu; barua iliyoandikwa mioyoni mwetu (na watoto wetu) kila mtu aione na kuisoma." (II Wakorinto 3:2).

Kumbuka: Darla Dillon ni mke, mama Mchungaji, mama wa watoto watatu, bibi kwa wajukuu watatu + mmoja yuko njiani. Pia kwa sasa hutumika kama Rais wa Wizara ya Wanawake wilaya ya British Columbia

Kamwe usisahau rasilimali tatu za nguvu daima kuwa zinapatikana na wewe: upendo, maombi, na msamaha. -H. J. Brown, Jr.

Kutoka kwa Mhariri

Debbie Akers

Mungu anatenda maajabu!

Imekuwa lengo langu na maono tangu mara ya kwanza kuulizwa kuanzisha jarida hili kwamba liwe linapatikana katika lugha mbalimbali. Mungu ni anafungua milango mingi na jarida hili sasa linapatikana kwa Kiingereza, Kihispania, Kifaransa, Kijerumani, Kiholanzi, Kireno, Kirusi, Kigiriki, Kiarabu, Kiajemi, Kicheki, Kichina, Kiswahili, Hungarian na Tagalog. Shukrani za pekee kwa Dada zangu Dianna Tuttle na Jerolyn Kelley na timu ya Watafsiri wanaofanya jambo hili liwezekane kila mwezi! Pia, Mchungaji Don Hanscom anashughulikia kutafsiri katika lugha ya Urdu, Hindi, Thai, Tamil, Kisinhali na Laotian! Hivyo chini ya uongozi wa Dada Gwyn Oakes, Raisi wa UPCI Ladies Ministry, kuwakilisha dhamira yetu ya maombi kwa ajili ya watoto wetu duniani kote bora, kuanzia sasa tutakuwa tukijulikana kama Wamama wa Maombi wa Kimataifa. Tunafuraha na tunazidi kumwomba Mungu aendelee kubariki huduma hii ya maombi. -Debbie Akers, Mratibu na Mhariri wa Wamama wa Maombi wa Kimataifa

Tafadhali tuma shuhuda na maombi kwa:
MothersOfPrayerIntl@aol.com or debiakers@aol.com

Wamama wa Maombi Kimataifa Ripoti kutoka France

Salamu, Ninataka kuwashukuru kwa ubora wa jarida hili. ninashiriki jarida hili na wanawake katika makanisa yote mawili ambayo tunachunga na wao hulisubiri kwa hamu kila mwezi. Hivi sasa natumia Kiingereza, Kifaransa, na Urusi. Nina furaha kubwa kuona kwamba sasa linapatikana katika Tagalog Filipino, pia!

Mungu awabariki – Wewe ni baraka kwa wamama wa Kikristo duniani kote! –Dada Darla Brochu, Mama Mchungaji, France

Wamama wa Maombi Kimataifa Ripoti kutoka Venezuela

Dada Akers,
Salamu katika Jina la Yesu. Wanawake wetu hapa nchini Venezuela wana msisimko juu ya Wamama wa Maombi na wameanza kuwa na mikutano maalum Jumamosi na akina mama kuomba kwa ajili ya watoto wao. Hivyo najaribu kila mwezi kutuma toleo la Kihispania kwa wanawake walio katika uongozi hapa ili waweze kuwapa wake wa mawaziri ambao wana jukumu katika makutano yao.

Shukrani. –Dada Gail Burton, Mmishenari kwenda Venezuela

Shuhuda

Nina furaha na shukrani mjukuu wangu, Madison Akers, (pichani kushoto) alibatizwa usiku wa Jumapili iliyopita! (Julai 6, 2014) -Debbie Akers

Kanisa letu lina furaha na linatoa shukrani kwa ajili ya mkono wa Mungu wa ulinzi wa mmoja wa vijana wetu wakike Alhamisi iliyopita, Juni 5. Grace anahudhuria Seattle Pacific University katika jiji la Seattle, ambapo mtu alikuja kwenye chuo hicho, na kuelekea katika moja wapo ya vituo vya wanafunzi mwanafunzi, na kuanza kupiga risasi. Kwa bahati mbaya, kabla ya yeye kushikwa na mwanafunzi, watu watatu walipigwa risasi na mmoja alifariki baadaye hospitalini. Grace alituambia, ingekuwa mtu huyo alienda chuo Jumatano au Ijumaa , kwa sababu ya ratiba yake ya darasa, naye angekuwa katika kituo hicho wakati wa mashambulizi hayo. Pia alituambia jinsi gani kikundi cha marafiki zake wa karibu wote walikuwa katika maeneo mbalimbali chuoni, au wamekwenda nyumbani, kama yeye, badala ya kuwa katika kituo hicho wakati huo. Mara moja nikakumbuka kumsikia mama yake katika sala kina ya maombezi wakati wa mkutano wetu wa MOPI sala siku chache tu kabla!

Pia tunataka kusema Asante, Wamama wa kanisa la Umoja la Pentekoste, kwa ajili ya kushikamana pamoja siku / jioni ile ya maombi. Kadri tunavyopata taarifa zaidi kuhusu mtu huyo, tunatambua kulikuwa na njia nyingi tukio hilo lingeweza kuwa la hatari zaidi kwa vijana wa mji wetu, na wale walio kwenye Vyuo Vikuu vinginevyo na shule. Hakuna shaka Maombi yalileta tofauti kwa mmoja wa binti zetu! - Leah Seagraves, Mama Mchungaji, SeaTac, WA

Amali 31 za Biblia za kuomba kwa ajili ya watoto wako (13-15)

13. Usafi - "Wape mioyo safi Ewe Mungu na hebu usafi huo wa moyo huonekane katika vitendo vyao." (Zab. 51:10)

14. Wema -. "Bwana, wawezeshe watoto wangu siku zote kujaribu kuwa wema baina yao na kwa wengine wote." (1Thess. 5:15)

15. Ukarimu -. "Wajalie watoto wangu waweze kuwa wakarimu na tayari kushiriki, na hivyo kujiwekea hazina kama msingi imara kwa wakati ujao." (1 Tim. 6:18-19)

Imewasilishwa na Gwyn Oakes. Hati miliki Bob Hostetler (www.bobhostetler.com). Imetumiwa kwa ruhusa ya mwandishi.

Kwa mengineyo

Pentecostal Publishing House
Mothers of Prayer Intl
UPCI Ladies Ministries
Reflections
Today's Christian Girl
More to Life Bible Studies
World Network of Prayer
UPCI
My Hope Radio
Multicultural Ministries

Kumbukumbu ya Wamama

Skani msimbo wa QR kwa taarifa juu ya Kumbukumbu ya Wamama

The Girl in the Dress (Msichana katika gauni)..... $10.00
PPH Hisa #: 22690 Lori Wagner

Kitu cha kusisimua! Hatimaye, kitabu kilichoandikwa tu kwa ajili ya wasichana - kitabu juu ya umuhimu na uzuri wa utakatifu. Kitabu hiki kinachoitwa Msichana katika gauni kitatusaidia kutambua ni kwa nini ni muhimu kuchukua msimamo katika dunia ya leo juu ya staha na usafi. Waandishi wamechukua mbinu bora juu ya jinsi Biblia inavyotufundisha kutembea, kuzungumza, na kuvaa.

Mpigie Jane wa UPCI Huduma ya Wamama katika 314-837-7304 X 412 kuweka oda yako leo!!